**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S. L.P. 38**
**GEITA**
**Simu: 028-2520004**
**Nukushi: (028) 2520040**
**Baruapepe:** rbcgeita@pccb.go.tz
**Website**: www.pccb.go.tz

**GEITA – JANUARI 15, 2021.**

## TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

## TAKUKURU MKOA WA GEITA YAOKOA JUMLA YA SHILINGI 141,558,150 NA KUTAIFISHA GARI AINA YA ESCUDO NA SIMU VILIYOTUMIKA KUTENDA MAKOSA YA RUSHWA

**NDUGU WANAHABARI**
Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia kibali cha kukutana siku ya leo. Aidha ninawashukuru ninyi wote kwa kuitikia wito kuja kushiriki mkutano huu kwa ajili ya kuuhabarisha umma juu ya kazi ambazo zimetekelezwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Nina washukuru wote kwa jinsi tulivyoshirikina katika Uchaguzi Mkuu 2020 na kapita salama. Karibuni sana ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Geita.

**NDUGU WANAHABARI**
Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 tumeweza kutekeleza majukumu ya Uchunguzi na Mashtaka, Uelimishaji umma juu ya Mapambano dhidi ya Rushwa, Uzuiaji Rushwa pamoja na Ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**NDUGU WANAHABARI**
***Uchunguzi na Mashtaka wa tuhuma za Rushwa*** umewezesha uokoaji wa fedha jumla ya shilingi **132,558,150/=** zilizofanyiwa ubadhirifu kwa njia mbalimbali za Rushwa, dhuluma na utapeli.

- Kiasi taslimu cha shilingi **11,750,000/=** ni fedha zilizorejeshwa kutokana na uchunguzi katika katika sekta ya Tamisemi, Elimu kwa mchanganuo ufuatao;

- Shilingi **350,000/=** zimetokana na uchunguzi wa mtumishi aliye staafu lakini aliendelea kupokea mshahara wa serikalini na fedha zimerejeshwa serikalini.
- Shilingi **400,000/=** ni fedha zilizookolewa kutokana na mishahara hewa katika sekta ya Elimu ambazo zimerejeshwa serikalini.
- Shilingi **11,000,000** zilizookolewa na kulipwa kwenye akaunti ya BAKATWA hii ni baada ya TAKUKURU kufanya uchunguzi na kubaini kuwa fedha hizi awali zilitaka kutapeliwa na kulipwa kwa mtu aliyejifanya Sheikh kumbe sio kweli na fedha hizi zilikuwa ni fidia ya makaburi ya waislam ambazo zilikuwa zinalipwa na halmashauri baada ya kuchukua eneo la BAKWATA.

- Kiasi cha shilingi **10,180,000/=** ni marejesho ya mikopo mbalimbali waliokuwa wanadaiwa wakopaji na kisha kushindwa marejesho ya fedha walizokuwa wanadaiwa na fedha hizi zilirejeshwa kwa wahusika.

- Kiasi cha shilingi **22,752,000/=** ni fedha ya deni alilokuwa wanadaiwa watuhumiwa baada ya kushindwa kulipa gharama za vifaa vilivyopelekwa kwenye kampuni zao.

- Shilingi **5,480,000/=** ni fedha zilizookolewa na kurejeshwa kwa Mwalimu kutokana na biashara ya mtandaoni ya Q-NET

- Shilingi **4,000,000/=** ni baadhi fedha zilizorejeshwa kwa mlalamikaji baada ya kuwa amempatia mtuhumiwa kwa lengo la kununulia kiwanja na kumjengea nyumba na mtuhumiwa alishindwa kutekeleza makubaliano hayo.

- Shilingi **2,550,000/=** ni fedha posho ambazo walimu walitakiwa kulipwa kwa kazi ya kusahihisha mitihani ya darasa la saba baada ofisi yetu kufatilia walimu husika walilipwa haki yao.

- Shilingi **14,976,150/=** ni fedha za mishahara ambazo walikuwa wamedhulumiwa wafanyakazi ishirini (20) wa kampuni ya Majaliwa Investment Co. Ltd na fedha hizi walirejeshewa wafanyakazi.

- Shilingi **9,000,000/=** alizokuwa amedhulumiwa na Bwana Obedi Mwita baada ya kuwa amemkopesha na akawa anamzungusha kumrudishia, baada ya fedha kurejeshwa alikabidhiwa mlalamikaji.

- Shilingi **3,000,000/=** ni baadhi ya fedha ambazo wanachama wa vikoba walikuwa wanamdai kiongozi wao wa vikoba na fedha hii ilirejeshwa kwa wana vikoba.

- Shilingi **16,250,000/=** ni fedha ambazo watuhumiwa walitakiwa kurejesha kwa wafugaji ambao waliwaaomba rushwa na hii ni amri ya mahakama baada ya watuhumiwa kukutwa na hatia ya kuomba na kupokea rushwa.

- Jumla ya Kiasi cha shilingi **1,020,000/=** fedha hizi zilirejeshwa kwa wananchi mbalimbali wa mji wa Geita baada ya kufanyiwa dhuluma na utapeli kwa watu wasiokuwa waaminifu.

- Jumla ya Kiasi cha shilingi **1,115,000/=** fedha za makato ya PSSSF ambazo wafanyakazi walikuwa wanakatwa na mwajiri lakini fedha haziwasilishi kwenye mfuko wa jamii wa PSSSF.

- Gari aina ya **ESCUDO** na Simu aina ya **TECNO** zilitaifishwa na kuwa mali ya serikali kwa amri ya mahakama baada ya mtuhumiwa kukutwa na hatia ya kuomba na kupokea fedha na vitu hivi vilivyotaifishwa vilitumika katika kutenda makosa ya rushwa.

- Viuwatilifu ambavyo ni dawa aina ya Duduba 450EC Box 19 sawa na chupa 1,900 zenye thamani ya shilingi Milioni Tisa na Laki Tano tu (shilingi **9,500,000/=**) zilikamatwa zikiwa zinatoroshwa kwenda Tabora katika upekuzi uliofanywa na maafisa wa Takukuru katika basi la KBS dawa hizi zilikabidhiwa kwa mwakilishi wa Bodi ya pamba mkoani Geita na viongozi wa AMCOS ya BUGAKA ili zikagawiwe kwa wakulima.

- Jumla ya Kiasi cha shilingi **28,945,000/=** ni fedha zilizookolewa baada ya kutaka kulipwa kwa Madiwani wa Halmashauri ya Nyanghwale lakini baada ya TAKUKURU kujiridhisha na nyaraka ilibaini kiasi kilichotakiwa kulipwa ni shilingi **3,415,000/=** na sio **32,360,000/=** na hivyo kuwa imeokoa tajwa hapo juu.

Katika kipindi hiki cha Oktoba hadi Desemba, 2020 pamoja na fedha zilizotemeshwa mikononi mwa mafisadi hawa, Taasisi imeweza kufungua mashauri manne (04). Jumla ya mashauri yaliyoendeshwa mahakamani ni 36 ambapo 13 yalitolewa maamuzi na Jamhuri kushinda mashauri 12 na kushindwa shauri 01.

Aidha katika kipindi husika jumla ya malalamiko dhidi ya rushwa na makosa mengine 113 yamepokelewa na kinara wa kulalamikiwa ni sekta ya Serikali za Mitaa malalamiko 42, Binafsi 33, Elimu 16, Fedha 16, Madini 08, Mifuko ya Jamii 8, Biashara 06, Afya 05, Polisi 05, Ardhi 05, Mahakama 03, Vyama vya ushirika 03, Misitu 03, Kilimo 02, Uchaguzi 02, Dini 02, Ujenzi 02, Maji 01, Siasa 01, Ulinzi 01, na Nishati 01.

Uchunguzi wa awali wa malalamiko haya umefanyika ambapo jumla ya majalada ya uchunguzi 14 yamefunguliwa, taarifa 01 imehamishiwa ofisi nyingine, taarifa 05 zimefungwa, taarifa 24 zilitolewa ushauri na hatua za kiutawala na taarifa 135 zinaendelea kufanyiwa kazi. Katika kipindi hicho jumla ya majalada 12 uchunguzi wake umekamilika na majalada 04 yamepelekwa kwa DPP kuombewa kibali cha mashitaka.

**NDUGU WANAHABARI**

Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 TAKUKURU imetekeleza jukumu la ***kuhamasisha umma kushiriki mapambano dhidi ya Rushwa*** kwani bila ushiriki wa dhati wa jamii nzima mapambano haya hayataleta tija iliyokusudiwa.

Tumeendelea kutumia mbinu mbalimbali za kuelimisha kupitia semina 35, mikutano ya hadhara 30 ikiwa ni sehemu ya kuelimisha wananchi kuchagua viongozi bora na sheria za uchaguzi na makatazo katika kipindi cha kampeni na uchaguzi mkuu 2020 pamoja na elimu ya kampeni ya UTATU, VUNJA UKIMYA KATAA RUSHWA YA NGONO na matumizi ya TAKUKURU APP, ufunguaji wa klabu za wapinga Rushwa 53 na uimarishaji wa klabu za wapinga Rushwa 85 katika Shule za Msingi na Sekondari, vipindi vya Redio 06, taarifa kwa vyombo vya habari 15, maonesho 07, mkutano na waandishi wa habari 03 na kugawa machapisho mbalimbali kwa wananchi.

**NDUGU WANAHABARI**

Kama nilivyoeleza awali kuwa majukumu mengine yaliyotekelezwa ni ***Uzuiaji Rushwa na Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa miradi ya maendeleo***. Katika uzuiaji rushwa lengo kubwa ni kufanya uchambuzi wa mifumo ya utendaji kazi ili kuziba mianya ya Rushwa kupitia warsha na matekelezo.

Katika kipindi hiki tumefanya uchambuzi wa mifumo katika Katika kipindi cha Oktoba hadi Desemba, 2020 tumefanya uchambuzi wa mfumo katika Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na madiwani uliofanyika 28 Oktoba, 2020 katika Majimb0 7 (Jimbo la Geita Mjini, Jimbo la Geita Vijijini, Jimbo la Busanda, Jimbo la Chato, Jimbo la Nyanghwale, Jimbo la Bukombe na jimbo la Mbogwe) ya Mkoa wa Geita , Uchambuzi wa Manunuzi ya Umma katika Halmashauri ya Mji wa Geita, Ukusanyaji wa ushuru wa huduma (Service Levy) katika Halmashauri na Huduma zinazotolewa katika vituo vya Afya katika vituo vya afya.

Aidha Ofisi imefanya warsha ya Manunuzi ya Umma katika Halmashauri ya Mji wa Geita, warsha katika utoaji wa Huduma katika vituo vya Afya na warsha katika ukusanyaji wa ushuru wa huduma (service levy).

Hata hivyo ofisi imechukua jukumu la kuandaa warsha kwa chambuzi ambazo hazikufanyiwa warsha pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio ya warsha kazi hizi zitakayofanyika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2021 ili kuweza kuweka mikakati ya pamoja na halmashauri, wasimamizi wa vituo vya afya na wadau mbalimbali ili kuwa na uelewa wa pamoja juu na kuboresha na kuondoa mianya ya rushwa katika utendaji kazi na kisha kuweka maazimio ya pamoja kwa muda maalum ya jinsi ya kuondoa mapungufu hayo.

Aidha miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi **5,602,894,067.72** imefuatiliwa katika sekta za Elimu, Maji, Maendeleo ya Jamii na Afya lengo likiwa ni kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa kuzingatia thamani ya fedha (value for money).

Miradi iliyofuatiliwa ni; Ujenzi wa bweni moja (1) Shule ya Sekondari Kalangalala shilingi 75,000,000/=, Miradi ya Makundi Maalumu ya Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu ya asilimia 10% ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Mji wa Geita shilingi. 919,025,000/= kwa vikundi 130 vya Halmashauri ya Mji katika Kata 15 za Halmashauri ya Mji wa Geita.

Miradi mingine iliyofuatiliwa ni; Ujenzi wa bwalo na mabweni mawili (2) Shule ya Sekondari Nyang'hwale shilingi 250,000,000/=, Ujenzi wa mradi wa maji katika vijiji 4 vya Nyugwa, Lushimba, Kafita na Mwamakiliga Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale. Shilingi. 83,955,326.72/=, Matumizi ya asilimia kumi (10%) ya Mapato ya Ndani kwa ajili ya makundi maalum (wanawake, vijana na walemavu) shilingi 1,183,525,340/= miradi ya maji (RUWASA) na ukamilishaji wa zahanati 10 Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale shilingi. 500,000,000/=

Miradi mingine iliyofuatiliwa ni wa matumizi ya asilimia kumi (10%) ya mapato ya ndani ya halmashauri ya wilaya ya Mbogwe kwa mwaka 2019/2020 iliyotengwa kwa ajili ya makundi maalum ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ambapo Halmashauri ilikopesha jumla ya Shilingi 86,748,400 /= kwa vikundi 50 na mradi wa ujenzi Hospitali ya Wilaya ya Mbogwe ambapo Halmashauri ilipokea shilingi milioni mia tano (500,000,000) kutoka serikali kuu kwa ajili ya kuanza kujenga majengo mawili (Jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na maabara) ya hospitali ya Wilaya Mbogwe na hadi sasa ujenzi umefikia asilimia sitini (60%).

Miradi mingine iliyofuatiliwa ni kiwanda cha kuchakata na kufaungasha mazao ya nyuki katika sekta ya viwanda mradi wenye thamani ya shilingi 435,000,000/= halmashauri ya wilaya ya Bukombe. Matumizi ya asilimia 10% ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya wilaya ya Bukombe kwa ajili ya makundi maalumu (wanawake, vijana na wenye ulemavu) thamani ya mradi ni Tshs 169,640,000/=

Miradi mingine iliyofuatiliwa ni ujenzi wa shule mpya ya sekondari ya Rubambangwe wenye thamani ya shilingi 700,000,000/= na mradi wa Ujenzi wa Shule mpya ya sekondari ya Mbuye wenye thamani ya shilingi 700,000,000/= katika halmashauri ya wilaya ya Chato.

**MWISHO**

Mikakati ya TAKUKURU Mkoa wa Geita kwa kipindi cha Januari – Machi, 2021 ni kuendelea kutatua kero za wananchi zinazohusiana na vitendo vya Rushwa na dhuluma za aina mbalimbali, kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kwa wananchi ili waelewe haki na wajibu wao, kuendelea kuwaelimisha watumishi wa sekta za Umma na binafsi kuwa waadilifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

Vilevile TAKUKURU Mkoa wa Geita imetenga siku moja kila mwezi ambapo itakuwa inawafuata wananchi walipo ili kusikiliza na kutatua kero zao dhidi ya rushwa. Kwa mwezi Januari tutasikiliza kero tarehe 28.01.2021 katika eneo la Katoro.

Aidha ni wito wa TAKUKURU mkoa wa Geita kwa watumishi wa umma mkoani humu kuzingatia kanuni na taratibu pindi wanapohitaji huduma za mikopo ili kuepukana na mikopo umiza kama nilivyoeleza hapo juu. Na wakopeshaji ni vyema wakazingatia kanuni za biashara ya ukopeshaji fedha maana kinyume na hivyo watakuwa wanatenda makosa ya jinai na wataendelea kuchukuliwa hatua za kisheria.

Wito wetu kwa wananchi wa mkoa wa Geita, waendelee kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, kuwa waadilifu kwa kutojihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa, washiriki pia kutoa taarifa za vitendo vya rushwa TAKUKURU kwa kupiga simu ya bure 113, *113# au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kwenda namba 113 au kupitia TAKUKURU APP.

**Sote Tuseme**

***"KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU"***

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**

**IMETOLEWA NA:**

**Azza Mtaita**

**KAIMU MKUU WA TAKUKURU (M) GEITA**